

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



16 Mtaa wa Urambo,
S. L. P 6420,
11102 Ilala,
DAR ES SALAAM.
TANZANIA.
Simu 022 – 2150043-7

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**MTAALAM WA MIONZI WA MOI NA AFISA UTUMISHI WA WIZARA YA ELIMU,
SAYANSI NA TEKNOLOJIA WAFIKISHWAMAHAKAMANI KWA MAKOSA YA
RUSHWA.**

Mtaalam wa mionzi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) Bwana Sirciacus Mwombeki, tarehe 31/01/2019 alikamatwa na maafisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kosa la kushawishi kuomba na kupokea rushwa kinyume na sheria.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ilala Bw. Christopher Myava alisema mtuhumiwa huyo anakabiliwa na makosa ya kushawishi, kuomba na kupokea rushwa ya Tsh laki tano (500,000/=), kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007.

Bw. Myava alieleza kuwa, mnamo tarehe 28/01/2019 bwana Mwombeki akiwa kwenye majukumu yake alishawishi, aliomba na kupokea shilingi elfu arobaini (40,000/=) ili aweze kumsaidia mtoto wa Kazembe Bundala (Nangale Kazembe) kwenye upasuaji wa uvimbe kwenye goti.

Mkuu wa Takukuru Ilala aliendelea kueleza kuwa tarehe hiyo 28/01/2019 Bwana Mwombeki alishawishi na kuomba shilingi milioni moja na laki tano (1,500,000/=) pamoja na mchele kilo kumi (10) ili aweze kumsaidia mtoto wa Kazembe afanyiwe upasuaji wa goti.

Mnamo tarehe 31/01/2019 mtuhumiwa Mwombeki akiwa kwenye majukumu yake MOI alipokea shilingi laki tano (500,000/=) kutoka kwa Kazembe Bundala kama sehemu ya malipo ya fedha iliyooombwa ili kumsaidia mtoto wa Kazembe kufanyiwa upasuaji wa goti.

Mtuhumiwa amefikishwa mahakamani leo tarehe 04/02/2018 katika mahakama ya Wilaya ya Ilala na dhamana ipo wazi, kesi hii itatajwa tena tarehe 18/02/2019 mbele ya Mheshimiwa Nasari.

Wakati huohuo

Takukuru Mkoa wa Ilala imemfikisha mahakamani bwana William Komba ambaye alikuwa Afisa Utumishi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa makosa ya kutumia madaraka vibaya kinyume na kifungu cha 31 cha sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007 na kuisababishia serikali hasara kinyume na Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi (Cap.200 R.E. 2002)

Bw. Komba alitumia madaraka yake vibaya akiwa anatekeleza majukumu yake kwa kuingiza jina la Yotham Buratwaye kwenye mfumo wa LAWSON payroll kinyume na utaratibu na kuisababishia serikali hasara ya shilingi 2,459,868.35/=

Mtuhumiwa amefikishwa mahakamani leo tarehe 04/02/2019 katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala na dhamana ipo wazi. Kesi hii itatajwa tarehe 18/02/2019 mbele ya Mheshimiwa Mpanze.

Imetolewa na Bw. Christopher Myava - MKUU WA TAKUKURU MKOA WA ILALA
04/02/2019